

Hatua za Kufanya Makadirio ya Kodi Kupitia Mfumo wa TRA Online

1. Tembelea Tovuti ya TRA

Nenda kwenye tovuti rasmi ya TRA: [www.tra.go.tz](#). Chagua sehemu ya Online Services kisha bofya "TRA Online TMS" au "Taxpayer Portal".

2. Ingia kwenye Akaunti yako ya TIN

Ingiza Username (Namba yako ya TIN) na Password ulizoweka wakati wa usajili. Kama huna akaunti, tafadhali jisajili kwa kubofya "Register".

3. Fungua Sehemu ya 'Return Processing'

Baada ya kuingia kwenye dashboard, chagua "Return Processing" kisha "Income Tax Return (ITR)" na hatimaye "Estimated Return (ITR - EST)".

4. Chagua Mwaka wa Kifedha

Chagua mwaka wa kifedha (mfano: 2025) kisha endelea na kujaza taarifa za makadirio yako.

5. Jaza Taarifa za Mapato Yanayotarajiwa

Ingiza taarifa za mapato yako ya mwaka mzima, ikiwa ni pamoja na aina ya biashara, kiasi cha mauzo au mapato, gherama za uendeshaji, na faida inayotarajiwa.

6. Angalia Makadirio ya Kodi

Mfumo utahesabu kiasi cha kodi utakachopaswa kulipa. Kiasi cha kodi kinategemea mapato yako, na kinagawanywa katika robo nne (quarterly payments).

7. Wasilisha Makadirio Yako

Hatua za Kufanya Makadirio ya Kodi Kupitia Mfumo wa TRA Online

Baada ya kujaza taarifa zote, bofya "Submit" ili kuwasilisha makadirio rasmi kwa TRA. Utapokea fomu ya makadirio (ITR-EST Form) kwa kumbukumbu zako.

8. Pakua Control Number na Lipa Kodi

Baada ya kuwasilisha, mfumo utakutengenezea control number kwa ajili ya malipo. Unaweza kulipa kodi kupitia benki, M-Pesa, Airtel Money, au kupitia online banking.